



**NAETISL**

National Association of  
Educational Translators and  
Interpreters of Spoken Languages



**MODDC**

Missouri  
Developmental  
Disabilities Council

# Kuelewa Majukumu ya Usalama wa Shule : Mwongozo wa Mzazi

---

Funding for the Supporting Language Access in Schools Project in Missouri provided by the Missouri Developmental Disabilities Council, was supported by the Administration for Community Living (ACL), U.S. Department of Health and Human Services (HHS) as part of a financial assistance award totaling \$1,361,246 with 100 percent funding by ACL/HHS. The contents are those of the author(s) and do not necessarily represent the official views of, nor an endorsement, by ACL/HHS, or the U.S. Government.



[naetisl@gmail.com](mailto:naetisl@gmail.com)



[www.naetisl.org](http://www.naetisl.org)

NAETISL



*Follow us*



MODDC



[moddc@moddcouncil.org](mailto:moddc@moddcouncil.org)



[www.moddcouncil.org](http://www.moddcouncil.org)





## Kuelewa Majukumu ya Usalama wa Shule : Mwongozo wa Mzazi

### Je, shule zina wajibu gani wa kisheria na kimaadili kuhusu usalama wa wanafunzi?

Shule lazima ziwalinde wanafunzi kutokana na madhara ya kimwili na kisaikolojia. Majukumu haya yanatokana na sheria za shirikisho na jimbo, pamoja na mbinu bora katika elimu na ustawi wa wanafunzi.

### Shule zinafaa kufanya nini kuhakikisha usalama wa kimwili?

- Hakikisha mazingira salama. Shule lazima zihakikishe kwamba majumba, madarasa, viwanja vya michezo, na usafiri vyote viko :
  - Salama na kutunzwa vizuri
  - Bila hatari za (k.m., moto, umeme , ama miundo msingi)
  - Kutii sheria za usalama na taratibu za dharura
- Kuwalinda wanafunzi kutokana na hatari za kimwili. Wafanyikazi lazima:
  - Wasimamie wanafunzi ipasavyo
  - Waingilie mapigano au tabia isiyo salama
  - Wajibu vitisho (k.m., silaha au vitu hatari)
  - Wafuate itifaki za majeraha, ugonjwa na dharura
- Jiandae kwa dharura. Shule lazima:
  - Iwe na mipango ya usalama kwa mioto, dharura za hali ya hewa, kufungwa kwa shule, na vitisho vinavyoendelea
  - Ifanye mazoezi ya mara kwa mara na kueledeleza mafunzo ya wafanyikazi
  - Iwasilishe taratibu za dharura kwa familia





## Shule zinapaswa kufanya nini ili kuhakikisha usalama wa kisaikolojia na kihisia?

- Zuia uonevu na unyanyasaji. Chini ya sheria ya shirikisho (pamoja na Kichwa IX na Sehemu ya 504), shule lazima:
  - Ifanye uchunguzi na kushughulikia uonevu, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji mtandaoni
  - Iwalinde wanafunzi dhidi ya unyanyasaji wa rangi, kijinsia, ulemavu, ama mambo mengine
  - Tekeleza sera za kupinga unyanyasaji na kutoa usaidizi kwa waathiriwa
- Toa usaidizi wa afya ya akili. Shule nyingi lazima
  - Ziajiri au kupata washauri, wanasaikolojia, au wafanyakazi wa kijamii
  - Zitoe marejeleo ya afya ya akili na uingiliaji kati wa shida
  - Zitoe usaidizi kwa wanafunzi walio na ulemavu wa kihisia au kitabia
- Kuhakikisha mazingira mazuri shuleni. Shule zinahimizwa ku:
  - Kukuza heshima, ushirikishwaji, na mwitikio wa kitamaduni
  - Tumia uingiliaji kati wa tabia chanya na usaidizi (PBIS)
  - Tekeleza programu za kujifunza kijamii na kihisia (SEL).

## Je, wanafunzi wenye ulemavu wanahitaji hatua za ziada za usalama?

Baadhi ya wanafunzi wanaweza kuhitaji usaidizi wa ziada wa usalama kwa sababu ya uhamaji, utambuzi, au masuala mengine. Hatua hizi zinapaswa kujadiliwa na kuandikwa katika IEP. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuhitaji usimamizi wa watu wazima nje ya darasa, au maelekezo ya ziada kuhusu kukaa salama katika jamii.





## Wazazi wanatarajia nini ama wanaweza kuomba nini?

- Sera zinazopinga uonevu na nidhamu
- Jibu la haraka kwa masuala ya usalama au vitisho
- Kushiriki katika kupanga tabia au usalama kwa mtoto wao
- Mawasiliano ya wazi wakati na baada ya matukio
- Marekebisho kwa watoto walio na kiwewe, wasiwasi, au mahitaji ya kitabia

## Wazazi wanapaswa kukumbuka nini ikiwa wana wasiwasi wa usalama?

Wazazi wana haki ya :

- Kuomba mkutano na wasimamizi wa shule
- Tuma malalamishi kwa wakala wa elimu wa wilaya au jimbo
- Tafuta utetezi au usaidizi wa kisheria ikiwa ni lazima

## Je, misingi ya kisheria ya usalama wa shule ni ipi?

- Kichwa cha IX (1972): Hulinda dhidi ya unyanyasaji au ubaguzi wa kijinsia shuleni.
- Kifungu cha 504 na Sheria ya Wamarekani Wenye Ulemavu: Huwalinda wanafunzi wenye ulemavu dhidi ya ubaguzi na uhakikisha kuwa kuna marekebisho yanayofaa.
- Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (IDEA): Inahitaji shule kushughulikia tabia zinazoingilia ujifunzaji kwa wanafunzi wenye ulemavu
- Sheria za serikali za unyanyasaji wa watoto: Inawaamuru wafanyikazi wa shule kuripoti unyanyasaji unaoshukiwa au kutelekezwa





- Sheria ya kesi: Mahakama inashikilia kuwa shule zinaweza kuwajibika ikiwa kwa makusudi hazijali vitisho vya usalama vinavyojulikana.

### **Wazazi wanawezaje kupata usaidizi kwa lugha yao?**

Omba huduma za mkalimani katika shule yam toto wako au katika ofisi za wilaya ya shule. Omba taarifa iliyotafsiriwa na kuandikwa iwapo utaihitaji. Taarifa inayopatikana kwa wazazi wote katika wilaya ya shule inafaa kupatikana kwako pia.

